**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU MURUTUNGURU**

Simu Na.0765418876/0787942375

S.L.P.68

Mail:*murutungurutc.@gmail.com*

NANSIO

Website:*http/www.murutungurutc.ac.tz*

**UKEREWE-MWANZA**

---

Ndugu..........................................................

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI MCHEPUO WA SAYANSI YA JAMII (KWA KUTUMIA LUGHA YA KISWAHILI) MWAKA WA MASOMO 2026/2027.**

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ninapenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na mafunzo ya **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi** mchepuo wa **Sayansi ya Jamii (Kwa kutumia Lugha ya Kiswahili)** katika **Chuo cha Ualimu Murutunguru** kwa mwaka wa masomo **2026/2027.** Chuo kinachukua wanachuo wa

**a)** Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa muda wa miaka miwili (02).

**b)** Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa muda miaka mitatu (03) **kwa njia ya masafa** (**Walimu Kazini).**

Yafuatayo ni maelekezo muhimu, yasome kwa makini na kuyazingatia.

**1. MAHALI CHUO KILIPO**

**Chuo cha Ualimu Murutunguru** kipo katika **Wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza**. Kipo umbali wa **kilometa 13** kutoka mji wa **Nansio** ambako ndiko makao makuu ya wilaya ya **Ukerewe**. Unaweza kuingia chuoni kwa njia zifuatazo: -

1. Kwa magari (basi) kutoka **Bunda hadi Nansio.**
2. Kwa meli kutoka **Mwanza hadi Nansio**. Usafiri upo kila siku kwa njia zote mbili.

2. **<u>KUFUNGUA CHUO</u>**

Unatakiwa ufike chuoni kuanzia **tarehe 17/08/2026 hadi 30/08/2026** bila kukosa.Baada ya hapo hautapokelewa kabisa utakuwa umepoteza nafasi yako na fursa ya mafunzo.

3. **<u>VIFAA VINAVYOHITAJIKA</u>**

**A: SARE KWA WANACHUO WA KAWAIDA.**

Wavulana: Njoo na: -

- Shati mbili (02) *Bluu Bahari* (light blue) mikono mirefu (tetron).
- Suruali mbili (2), moja nyeusi na bluu nyeusi moja (dark blue) zenye marinda mawili, zisiwe za kubana (upana chini usipungue **inchi** 14) na mkunjo chini (turn up).
- Koti mbili (2) moja nyeusi na bluu nyeusi (dark blue) moja za kushonwa lenye kitambaa sawa na suruali (lisiwe la mtumba) na liwe na mipasuo miwili.
- Jozi mbili (2) za viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza na kufunika kisigino na vyenye soli fupi.
- Tai mbili (2) nyeusi moja na blue nyeusi (dark blue) moja ndefu yenye kitambaa sawa na suruali na koti.
- Soksi nyeusi jozi mbili (2).
  NB: ***Kitambaa kiwe 'GRADE ONE'***

Wasichana: Njoo na: -

- Shati mbili (2); *light Blue* (tetron) mikono mirefu.
- Sketi mbili (2) nyeusi moja (01) na bluu nyeusi (dark bue) moja (01) za heshima ziwe rinda boksi zenye. urefu usipungue **sm 30** kutoka kwenye goti
- Jozi mbili (2) za viatu vyeusi vya kutumbukiza kisigino vyenye soli fupi. (***Simple shoes*** **haziruhusiwi**)
- Koti mbili (02) jeusi moja na buu nyeusi moja ya kushonwa lenye kitambaa sawa na sketi.
- Tai mbili (2) nyeusi moja (01) na blue nyeusi (dark blue) moja kitambaa sawa na sketi na koti.
- Soksi nyeupe jozi mbili (02) ndefu.
- Juba mbili (2) *light blue* kwa ***waislamu tu.***
  NB: ***Kitambaa kiwe 'GRADE ONE'***

**B: VIFAA VYA MICHEZO.**

Wavulana: Njoo na: -

- Jezi jozi moja (1) ya michezo***Taifa Stars*** bluu (T-shirt na bukta yake).
- Soksi za *stocking* za bluu zenye fito nyeupe.
- Raba za michezo rangi yoyote.
- Jozi moja (1) ya *truck suit* rangi ya bluu
- Vifaa vingine vya michezo utakavyoona vinafaa.
- T-shirt ya kijivu (Form Six) yenye nembo ya chuo itapatikana chuoni baada ya makubaliano ya gharama zake.

Wasichana: Njoo na: -

- Jezi jozi moja **(1) ya michezo ya *Taifa Stars* bluu (T-shirt na bukta yake).**
- Sketi **moja (1) fupi rangi yoyote.**
- Raba za michezo rangi yoyote.
- Jozi **moja (1) ya *truck suit*** rangi ya bluu.
- Vifaa vingine vya michezo utakavyoona vinafaa.
- **T-shirt ya kijivu** (**Form Six**) yenye nembo ya chuo itapatikana chuoni baada ya makubaliano ya gharama zake.

**C: <u>VIFAA VYA MALAZI</u>**

Chuo kitakupatia kitanda. Hivyo, njoo na: -

- **Godoro lako futi mbili na nusu ($2^1/_2$) kwa sita (6).** Kwa wanachuo watakaowahi yapo machache ya kukodi.
- **Blanketi moja (1).**
- **Shuka mbili (2) *light blue*** zisizo na maua ya kutarizi na foronya zake.
- Mto mmoja (1).
- **Chandaru (1)**

**D: <u>VIFAA VYA CHAKULA</u>**

Njoo na: -

- **Bakuli moja (1**), **sahani moja (1), kikombe kimoja (1)** na **kijiko kimoja (1)**
  NB: **Vyombo hivi visiwe vya plastiki!**

**E: VIFAA VINGINEVYO**

Njoo na **ndoo moja (1)** kwa ajili ya maji ya matumizi yako binafsi na **galoni ya lita tano(5**) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.

- **Jembe lenye mpini wake.**

**F: VIFAA VYA MASOMO**

Fika na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya masomo: -

- Madaftari makubwa ya kutosha masomo yote (**Counter Book Quire 3).** Yasipungue kumi.
- **Kalamu za wino (bluu/ nyeusi tu).**
- Kalamu za risasi.

G: **MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI**

Ili uweze kusajiliwa na kuwa mwanachuo halali sharti uje na: -

- Vyeti vyako halisi vya taaluma (**original academic certificates**), ***result slip*** au hati ya matokeo (***statement of results***) ya kuhitimu elimu ya sekondari kidato cha sita. (Kwa waliohitimu ngazi hiyo)
- Cheti cha **Ualimu Daraja A au *Statement of results*** na/au result ***slip*** (Kwa waliohitimu mafunzo ya ualimu ngazi ya Astashahada)
- Cheti au vyeti vyako halisi vya kumaliza elimu ya sekondari/ualimu. {**Leaving certificate(s**)} kwa ngazi zote za elimu ulizopitia.
- Cheti cha Kuzaliwa **(Birth Certificate**).
- Hati ya daktari kwa ajili ya uthibitisho wa afya yako.
- **Kadi ya bima ya afya.**
- Jarada bapa (flat file) moja (1) la kutunzia kumbukumbu zako.
- Risiti halisi za malipo za benki ***(Original bank pay -in-slip***) na nakala moja kwa kila satakabadhi ya michango na ada. Ada utalipa baada ya kupatiwa namba ya kumbukumbu ya malipo (***control number***) na chuo kupitia ofisi ya uhasibu. **USIJE NA FEDHA TASLIMU!**
- Kitambulisho cha taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya **Taifa (NIDA)** au namba ya kitambulisho cha utaifa **(National Identification Number-NIN).**
- Ream moja (1) **A4 *Double A*** ya karatasi nyeupe kwa ajili ya shughuli za kitaaluma.

**MUHIMU:** *Endapo utawasili chuoni bila kuwa na vyeti vyako halisi vya taaluma (original academic certificates), Result slip au hati ya matokeo (statement of results) ya kuhitimu elimu ya sekondari* ***HAUTAPOKELEWA*** *wala* ***HAUTASAJILIWA.***

**H: (I) ADA NA MICHANGO KWA WANACHUO WA KAWAIDA.**

| **AINA YA MALIPO** | **KIWANGO** | **NAMBAYA AKAUNTI /MAELEZO** | **JINA LA AKAUNTI** |
|---|---|---|---|
| **ADA** | **450,000/=** kwa mwaka | Piga simu kwa nanmba hizi kupata **control number. 0620734629/ 0689025101/ 0754896628** | |
| **MICHANGO** | 1. **Usajili na kitambulisho 20,000/=** mwaka wa kwanza tu.<br>**2. Ulinzi 30,000/= kwa mwaka**<br>3. **Ukarabati 25,000**/= kwa mwaka<br>4. **Usafi na mazingira 20,000/= kwa mwaka**.<br>5. **Michezo 30,000/= kwa mwaka**.<br>6. **Huduma ya kwanza 10,000/= kwa mwaka**.<br>7. **Serikali ya wanachuo Murutunguru (SEWAMU) 5000/= kwa mwaka**.<br>**8. Kukodisha godoro 10,000/= kwa mwaka.** | Lipa michango ya chuo katika akaunti namba ifuatayo: - **31401100001 NMB.** | PRINCIPAL MURUTUNGURU TTC |
| | **150,000/= Kwa mwaka** | | |

**H. (II) ADA NA MICHANGO KWA STASHAHADA YA NJIA YA MASAFA.**

a) **Ada ni Tsh 450,000/= kwa mwaka inalipwa kwa kupewa control namba na mhasibu kama maelekezo yalivyo hapo juu.**

b) Mchango wa Usajili 20,000/= kwa mwaka.

c) Mchango wa ufuatiliaji na uendeshaji wa mafunzo 40,000/= kwa mwaka.

d) Mchango wa fedha ya taaluma Tsh 60,000/= kwa mwaka.

e) Mchango wa ukarabati endelevu Tsh 25,000/= kwa mwaka.

f) Mchango wa serikali ya wanachuo Tsh 5000/= kwa mwaka.

**Jumla ya michango yote ni Tsh 150,000/=**

**NB.** Lipa michango ya chuo katika akaunti namba ifuatayo: - **31401100001NMB. Jina la Akaunti PRINCIPAL MURUTUNGURU TTC.**

**I: SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO**

Pamoja na kukidhi vigezo vya kusajiliwa na kuwa mwanachuo halali, mwanachuo atatakiwa kusoma sheria, kanuni na taratibu za chuo mara tu afikapo chuoni na hatimaye atajaza fomu ya kukubali na kutii sheria, kanuni na taratibu hizo.

**NYONGEZA:**

*Chuo hakipokei **fedha taslimu wala hundi (CHEQUE)** michango yote inalipwa kwenye akaunti husika. Unapaswa kukamilisha malipo ya ada na michango ndipo usajiliwe.*

*Kwa wale ambao vyeti vyao bado havijatolewa na **Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA)** njoo na karatasi ya matokeo (**result slip au statement of results**) iliyotolewa na **Baraza la Mitihani la Tanzania.** Aidha, unatakiwa kukata au kuja na bima yako ya afya. **Ni muhimu sana.***

*Kama una tatizo la kiafya (ugonjwa) kuwa wazi kuhusu ugonjwa huo, njoo na uthibitisho wa daktari kuhusu tatizo/ugonjwa ili chuo kione namna ya kukuhudumia kulingana na tatizo/ugonjwa huo. **KAMWE USIFICHE UGONJWA**.* **Kwa mawasiliano zaidi piga:**

- **0745 954 401 / 0622 144 401 Msajili wa wanachuo**
- **0759 358 832/0621134057 Mratibu wa Masuala ya Wanachuo**
- **0713 356 947/ 0755 432 991 Mratibu wa Masuala ya Taaluma**

G.G. MOTIBA

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MURUTUNGURU
S.L.P. 68 NANSIO

**KIAMBATISHO A: FOMU YA KUPIMA AFYA *(Ijazwe na daktari na kugongwa muhuri)***

**THE GOVERNMENT OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:** From: Murutunguru Teachers' College

TO: The Medical Officer

.......................................................................

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time teacher course.

A: 1. (a) Eye- sight (b) Hearing

(c) Speech (d) Venereal Diseases

(e) Leprosy (f) Limbs

(g) Epilepsy

2. Neuroses

3. Other serious Diseases

B. Blood Group

Date.................................

Signature.................................. Official Stamp

---

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above-named student that he/she is physically fit/ unfit and mentally *fit/unfit for a full time Teacher Education course

Eye Sight.......................................................................................................

Hearing............................................................................................................

Limbs..............................................................................................................

Speech.............................................................................................................

Leprosy...........................................................................................................

Neuroses.........................................................................................................

Other serious Diseases.....................................................................................

Pregnancy (Girls)..............................................................................................

Date: ............................................................ Signature.........................................................

Official Stamp